## Information about your rights while you are on a Community Treatment Order

## (Taarifa kuhusu haki zako unapokuwa kwenye Taratibu ya Tiba ya Jumuia)

**Ukiitaji msaada wa kuelewa kijitabu hiki, ao matibabu yako, tafadhali uulize wafanyakazi wakati wowote**

### What is a Community Treatment Order?

### (Taratibu ya Tiba ya Jumuia ni nini?)

Taratibu ya Tiba ya Jumuia ni njia ya kisheria ya kutoa tiba kwa mgonjwa wa akili wakati yeye hawezi kukubaliana na matibabu na ikiwa inaweza kuhatarisha usalama.

### What does it mean if I am on Community Treatment Order?

### (Inaimarisha nini ikiwa nipo kwenye Taratibu ya Tiba ya Jumuia?)

Ikiwa upo kwenye Taratibu ya Tiba ya Jumuia unahitajika kupata matibabu kwa magonjwa yako ya akili kwenye nafasi maalum na kwa vipindi vya kawaida.

Utapata aina mbalimbali ya matibabu, ambayo ni uakikisho mshinji bora zaidi kwa ugonjwa wako wa akili. Matibabu ni pamoja na majadiliano tiba, dawa na shughuli zingine.

Matibabu yatatolewa na wataalamu waliopata majifunzo za afia kama vile madaktari, manesi, wataalamu wa shughuli, wafanyakazi wa jamii na wanasaikolojia. Hawa wataalamu wa kazi watatumika pamoja na wewe ili kukusaidia kupona. Unaweza kujadili kuhusu matibabu yako wakati wowote na wataalamu ambao wanakusaidia.

Kama hauwezi kukubaliana na suala la Taratibu ya Tiba ya Jumuia na/ao ugonjwa wako wa akili hauboreki, unaweza kupendekezwa kuendelesha taratibu ya tiba ukiwa umelazwa, hiyo itakuomba kukaa hospitalini.

### Children Under 16 Years Old

### (Watoto chini ya miaka 16)

Ikiwa una miaka chini ya 16 basi mzazi ao mlezi anaweza kutumia haki zote kwa niaba yako.

### What are my rights when I am on a Community Treatment Order?

### (Haki zangu ni gani ninapokuwa kwenye Taratibu ya Tiba ya Jumuia?)

Wewe na msaidizi wako ikiwezekana) mutapokea nakala ya Taratibu na Taarifa za Haki haraka iwezekanavyo.

Unaweza kuwa na msaidizi wakati wa uchunguzi na matibabu, kwenye kipindi cha matibabu ginsi ilivyopangwa na timu ihusikayo na matibabu. Msaidizi wako anaweza kuwa mlezi, wakala wa matibabu, jamaa, mwangalizi, rafiki ao wakili hiari ao wa kikazi.

Matibabu yako na huduma vitaongozwa na Tiba ahueni pia Mpango wa Ulinzi. Wewe na msaidizi wako (ikiwezekana) mutashiriki kwenye maandalizi na ukaguzi wa mpango kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo.

Unaweza kuwa na mkalimali wa kukusaidia ikiwa una magumu ya Kingereza.

Unaweza kupata maoni mengine kutokea kwa mwanasaikayatria kuhusu utambuzi na chaguzi za matibabu.

Ikiwa hauridhiki ya kwamba matatizo yako hayakuzingatiwa, unaweza kupeleka malalamiko yako rasmi. Namba za simu za huduma ambazo zinaweza kukusaidia upatikana kwenye kijitabu hiki.

Unaweza kukata rufaa dhidi ya Taratibu ukiuliza Bodi ya ulinzi ili kuchunguza kesi yako. Watu wengine wanaweza pia kukata rufaa kwa niaba yako, ikiwa pamoja na msaidizi wako ao wakili. Unaweza kuomba Bodi ya ulinzi kutofautisha Taratibu yako wakati ipo chini ya rufaa.

Ukitaka kukata rufaa, tafadhali uulize taarifa kwa timu yako ya matibabu ginsi gani uataanza. Wakati wa maendelesho ya rufaa, unaweza kujiakilisha, ao msaidizi wako, ao mwanasheria wa kulipwa ao kuwa na mwanasheria anayelipwa na Idara ya Afya na Kuzeeka.

Wewe na msaidizi wako (ikiwezekana) mutapokea nakala za Taratibu yeyote ao maamuzi yaliofikiwa na Bodi ya ulinzi haraka iwezekanavyo.

Taarifa inayokuhusu ni siri alakini inaweza kutolewa ikiwa sheria inalazimisha, kwa ajili ya kupana huduma ao kwa kulinda usalama. Taarifa inaweza pia kutolewa kwa shirika nyingine, ao jamaa, mlezi ao rafiki ikiwa inatakiwa kabisa kwa ajili ya matibabu yako na huduma zinazoendelea na ni kwa maslahi yako bora.

## Advocacy (Utetezi)

Wakati mwingine wewe ao familia yako uhitaji msaada wa kuelewa mfumo wa afya ya akili.

**Peer Worker (Mfanyakazi wa rika)**
Kituo cha matibabu chaweza kuwa na Wafanyakazi wa rika ao Wataalamu wa rika ambao wanaweza kukusaidia. Tafadhali uulize wafanyakazi kwa taarifa zaidi. Mshauri Mlinzi pia anaweza kupatikana ili kusaidia walezi na familia.

**The Office of Public Advocate**
**(Ofisi ya Wakili wa Umma)** ni chombo huru ambacho ushauri, usaidia na kutetea watu wenyekupugukiwa na akili.
Simu: 08 8342 8200 Ita kwa bure: 1800 066 969

**The Disability Advocacy and Complaints Service of South Australia**
**(Huduma ya Utetezi Ulemavu na Malalamiko ya Australia ya Kusini)** ni mpangilio usio wa serikali unaosaidia na utetezi pia malalamiko za watu wenye ulemavu wa aina yeyote.
Simu: 08 8297 3500
Kuita bure inchini: 1800 088 325

**MALSSA** ni mpangilio usio wa serikali unaotetea wateja wa mfumo wa afya ya akili, hasa wale wa kutoka kwenye inchi isio ya Kingereza wakizungumza kwa utamaduni na kabila za asili mbalimbali.
Simu: 08 8351 9500

## Language Assistance (Msaada wa Lugha)

**Interpreting and Translating Centre (Senta ya Ukalimali na Utafsiri)**
Simu: 08 8226 1990
**Translating and Interpreting Service (Huduma ya Utafsiri na Ukalimali)**
Simu: 131 450 (Ya Kitaifa)

**National Relay Service (Huduma ya Relei ya Taifa)**
Kwa magumu ya kusikia na kuzungumza).
Simu: 133 677 Kuita bure: 1800 555 677

## Complaints (Malalamiko)

**Treatment Centres (Vituo vya Matibabu)** vina maafisa ambao wanaweza kusaidia kwa maoni na malalamiko. Tafadhali uulize wafanyakazi ili wakusaidie kuhusiana na mtu anayestahili.

**The Chief Psychiatrist (Mkuu wa ugonjwa wa akili)** uimarisha usalama na ufanyizi wa huduma za afya ya akili.
Simu: 08 8226 1091

**The Health and Community Services Complaints Commissioner (Kamishna wa Malalamiko za Huduma wa Afia na Jumuia)** usaidia kutatua malalamiko.
Simu: 08 8226 8666
Yasio malipo: 1800 232 007

© Department of Health and Ageing, Government of South Australia. All rights reserved. Printed June 2012

Government of South Australia
SA Health

# Taarifa Za Haki

## Community Treatment Orders

## Taratibu za Tiba za Jumuia

Office of the Chief Psychiatrist

Ofisi ya Mkuu Mwanasaikayatria

KISWAHILI

Government of South Australia
SA Health